



TAARIFA KWA VYOMBO HABARI

UTEKELEZAJI WA MRADI WA UKAGUZI NA UKUSANYAJI WA ADA ZA USIMAMIZI WA TAKA ZA KIELEKTRONIKI KWA VIFAA VYA MAWASILIANO VINAVYOINGIZWA NCHINI

Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) ni taasisi ya serikali iliyoanzishwa kwa sheria ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania Na. 12 ya Mwaka 2003. TCRA imepewa jukumu la kusimamia Sekta ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Lengo la TCRA ni kuboresha maisha ya Watanzania kupitia usimamizi bora wa sekta ya mawasiliano kwa kuwezesha ubunifu na kuhakikisha mawasiliano kwa wote kwenye huduma za mawasiliano salama, bora na nafuu.

Kwa kuzingatia mahitaji ya kifungu 5(1)(f) cha sheria ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (SURA ya 172 kama ilivyoboreshwa), TCRA katika kutekeleza kazi zake inalojukumu la kuhakikisha inaboresha maisha ya jamii ya watanzania kwa kutambua umuhimu wa kulinda na kutunza mazingira. Aidha, kwa kuzingatia kifungu 83(4) cha sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (SURA ya 306 kama ilivyoboreshwa Mwaka 2019), TCRA inajukumu la kusimamia vifaa vya mawasiliano ya kielektroniki pale vinapofika mwisho wa matumizi.

Kanuni za Uboru wa vifaa vya Mawasiliano ya Kielekitroniki na usimamizi wa Taka za Kielekitroniki za Mwaka 2020 zinatoa wajibu kwa wadau wanaohusika kwenye usimamizi wa wa vifaa vya mawasiliano ya kielekitroniki pale vinapofika mwisho wa matumizi wakiwemo watengenezaji, waingizaji, wanaokaranati pamoja na watumiaji wa vifaa vya mawasiliano ya kielekitroniki. Wajibu huo ni pamoja na:-

- a) Kuhakikisha kuwa vifaa vya mawasiliano ya kielektroniki ambavyo vimefika mwisho wa matumizi vinapelekwa kwa watoa huduma wenye leseni za kukusanya, kukarabati au kuendesha mitambo ya kuchakata vifaa vya mawasiliano vya kielektroniki pale vilivyofika mwisho wa matumizi;
- b) Kusajili kwa TCRA taarifa zote za vifaa vya mawasiliano ya kielektroniki ambavyo vimeingizwa au kutengenezwa nchini;
- c) Kushiriki kwenye mipango ya kupeleka elimu kwa umma kuhusu usimamizi wa taka za kielektroniki kupitia machapisho, mipango ya kukusanya vifaa vilivyo fika mwisho wa matumizi au njia nyingine za mawasiliano;

- d) Kulipa ada za usimamizi wa taka za kielektroniki kwa ajili ya kusimamia vifaa vya kielektroniki vinapofika mwisho wa matumizi;
- e) Kuweka makubaliano na watoa huduma waliopewa leseni kwa ajili ya kukusanya, kukarabati au kuendesha mitambo inayochakata taka za kielektroniki;
- f) Kuhakikisha kuwa vifaa vya mawasiliano vya kielektroniki vinavyoingizwa nchini havijafika mwisho wa matumizi;

HIVYO, TCRA inapenda kuujulisha umma, kuwa mtu binafsi au kampuni yeyote inayotaka kuagiza vifaa vya mawasiliano ya kielektroniki kuwa kuanzia tarehe 23 Mei 2023, vifaa vya mawasiliano ya kielektroniki vinavyoingizwa nchini vitatakiwa kukagulia kwenye nchi vinakoagizwa ili kuhakiki kuwa havijafika mwisho wa matumizi. Aidha, ada za usimamizi wa taka za kielektroniki italipwa kwa kila kifaa kinachoingizwa kwa ajili ya gharama za usimamizi wa vifaa hivyo vinapofika mwisho wa matumizi kama inavyoelekezwa na Kanuni za Uboru wa vifaa vya Mawasiliano ya Kielektroniki na usimamizi wa Taka za Kielektroniki za Mwaka 2020.

KATIKA KUTEKELEZA jukumu hili TCRA imeingia kandarasi na Kampuni ya M/S BUREAU VERITAS TANZANIA LIMITED kwa ajili ya kufanya ukaguzi wa vifaa vya mawasiliano ya kielektroniki kwenye nchi vinakoagizwa ili kuhakiki kuwa vifaa hivo havijafika mwisho wa matumizi pamoja na kuwezesha ukusanyaji wa ada za usimamizi wa taka za kielektroniki.

HIVYO, kuanzia tarehe 23 Mei 2023, maombi yote ya kuingiza vifaa vya mawasiliano ya kielektroniki yatawasilishwa kwa njia ya mtandao kupitia <https://verigates.tcra-bureauveritas.co.tz> ili kuwezesha uwasilishwaji wa taarifa zote za vifaa vinavyoagizwa. Baada ya maombi kupokelewa, uchambuzi tathmini kuhusiana na vifaa vinavyoagizwa pamoja na ada za usimamizi wa taka za kielektroniki itafanyika ili kuruhusu hatua zinazofuata kutekelezwa.

TCRA inapenda kuukumbusha umma kuwa uingizwa wa vifaa vya mawasiliano nchini unahitaji leseni tofauti yaani "*Importation License*"; na vifaa vyote vya mawasiliano ya kielektroniki vinavyoingizwa nchini vinatakiwa kuhakikiwa ili kutathmini ulinganifu na mwingiliano wakati wa matumizi.

IMETOLEWA NA

Mkurugenzi Mkuu,
Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania,
20 Barabara ya Sam Nujoma,
S. L. P 474,
14414 DAR ES SALAAM.
Simu: +255 22 241 2011-2
Nukushi: +255 22 2412009
Barua pepe: dg@tcra.go.tz

30 Machi 2023